

Mwingiliano wa Kanuni za Kimofosintaksia wa Ngeli Nomino za Luganda katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu

Martin Mulei¹, Beverlyne Asiko Ambuyo² na Debora Nanyama Amukowa²

¹Chuo Kikuu cha Kabale

²Chuo Kikuu cha Maseno

Ikisiri

Makala haya yanalenga kuweka wazi mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia wa ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti huu unatokana na tafiti za awali zilizobainisha kuwa Kiswahili kinachozungumzwa na kuandikwa na Wanauganda ni kile kinachokiuka kanuni na miundo ya kisarufi ya Kiswahili sanifu. Aidha, Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za Kibantu ambazo hutumia mfumo mmoja wa uianishaji wa ngeli, na uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya ngeli kimofosintaksia huweza kusababisha mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti. Data ya makala haya yalitokana na uchanganuzi wa mazungumzo na maandishi ya wanafunzi 117 wa shule za upili 15 teule wilayani Kampala, Uganda ambao L1 ni Luganda. Utafiti huu uliongozwa na mihimili ya usarufi bia na upatanifu wa nadharia ya Umilikifu na ufungamanisho (Chomsky, 1981) ambayo hudhihirisha hali ya vipashio fulani vya kisarufi kutawala na kumiliki vipashio vingine katika tungo. Kupitia kwa mijadala, usaili, uandishi na usimulizi wa insha na mijarabu ya kisarufi, matokeo yalidhihirisha wanafunzi kuhamisha, kuchanganya, kubadilisha, kuongeza na kujumlisha kanuni za kimofosintaksia za matumizi ya ngeli katika maandishi na mazungumzo ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwaongoza walimu na wanafunzi wa Kiswahili kutambua mchango wa lugha asili katika matumizi, ujifunzaji na ufundishaji wa L2, kutofautisha kanuni za Luganda na Kiswahili sanifu na athari zake katika Kiswahili sanifu na uimarishaji wa matumizi ya Kiswahili sanifu.

Maneno Muhimu: *Mwingiliano, kanuni, mofosintaksia, ngeli, nomino, Kiswahili*

Utangulizi na Mapitio ya Maandishi

Ngeli ni majina ambayo hupatikana katika kundi moja yaliyo na upatanishi wa kisarufi na viambishi ngeli vya idadi ya umoja na wingi unaofanana (TUKI, 1990, Kapinga, 1983). Mwingiliano wa kanuni za matumizi ya ngeli nomino katika matumizi ya Kiswahili sanifu ni athari za taratibu za matumizi ya ngeli za Luganda zinazojitokeza katika matumizi ya ngeli za Kiswahili kama kipashio cha kimofosintaksia. Licha ya kuwa matumizi ya ngeli huzingatia utaratibu wa kupanga nomino kuonyesha upatanishi wa kisarufi wa nomino na maneno mengine ya kategoria za kisarufi kimofolojia na kisintaksia, uwiano na tofauti za utaratibu wa uianishaji wa ngeli baina ya lugha asili na Kiswahili sanifu umeripotiwa kuwa kikwazo katika ufundishaji, ujifunzaji na matumizi ya Kiswahili sanifu (Ontieri, 2016).

Utafiti huu unachunguza mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia wa ngeli za Luganda katika Kiswahili sanifu. Wajifunzaji wa Kiswahili kama L2 huathiriwa na L1 kutokana na uwiano na tofauti za mifumo ya lugha asili na ule wa Kiswahili. Matumizi yanayopotosha usanifu wa lugha anayojifunza na kutumia mwanafunzi hutokana na maingiliano ya mifumo tofauti ya L1 na L2. Aidha, pana uwezekano kwamba mtumiaji lugha ya Kiswahili sanifu, asiye na ujuzi, huweza kuathiri lugha hii kwa miundo na mifumo ya lugha ya mama. Hii ni kwa sababu lugha mbalimbali huzingatia mifumo tofauti na wajifunzaji lugha huweza kuhamisha tajiriba ya L1 katika lugha ya pili kwa lengo la kurahisisha ujifunzaji wao (Mukuthuria 2008, Odeo na Maina, 2008). Katika kutumia mkakati huu, sifa za lugha lengwa anayojifunza na kutumia mwanafunzi hupoteza sifa zake kutokana na kutofautiana na kufanana kwa mifumo ya lugha hizo. Aidha, upotovu huu pia unaweza kutokana na ukuruba na upekee fulani wa lugha hata kama ni za nasaba moja. Kwa hivyo, pale lugha mbili za Kibantu zinapotofautiana kwa viashiria vya kimofimu, bila shaka kuathiriana kutakuwepo.

Makala haya yanachunguza mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia za ngeli za Luganda katika Kiswahili sanifu kudhibitisha kuwa athari za mwingiliano wa lugha hazijitokezi tu katika lugha zenye mifumo tofauti bali hata zile ambazo zina mifumo inayofanana na ambazo zinatoka katika nasaba moja kama ilivyo Luganda na Kiswahili. Luganda ni lugha nasibu yenye mifumo ya kipekee ya fonolojia, mofolojia na sintaksia inayotofautiana na lugha zingine za kibantu kama ilivyo Kiswahili sanifu (Hyman na Katamba (2001) na Katamba (2006). Tofauti za kiisimu kati ya Luganda na Kiswahili kimatumizi kupambanua upekee wa lugha hizi zilizo na ukuruba na mtagusano wa miaka na mikaka haujulikani. Kwa hiyo makala haya *yanaweka wazi mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia wa ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu*. Data ilichunguzwa kutoka kwa maandishi na mazungumzo ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita katika shule za upili wilayani Kampala, Uganda. Uchunguzi huu unatokana na kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hushirikisha kanuni za kimofosintaksia katika matumizi ya vipashio vya kisarufi kuunda tungo zenye dhamira za kisarufi hasa ngeli nomino. Aidha, *Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za kibantu ambazo zina mifumo ya matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia zinazofanana na kutofautiana, na tofauti hizi husababisha athari za mwingiliano wa kanuni za vipashio vya kimofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu*.

Tafiti mbalimbali zimeonyesha changamoto za ujifunzaji, ufundishaji na matumizi ya lugha ya pili. Miongoni mwa changamoto ikiwa mwingiliano wa L1 katika L2 katika viwango anuwai. Mukuria (1987) alilinganisha mpangilio wa ngeli za Kikikuyu cha Kiambu na Kiswahili sanifu. Ulinganishi wake ulijishughulisha na uainishaji wa ngeli za Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu kimuundo na kisemantiki kuzingatia vigezo vya idadi za ngeli, wiano wa kisarufi, na misingi ya kimaana inayotokea katika ngeli za lugha hizo. Utafiti wake ulitambua kuwa kimuundo kiambisho kilichoko kwenye jina hukaririwa kwenye vipande vingine vya sarufi ambavyo hutawaliwa na jina. Aidha, kisemantiki, Kila mojawapo ya ngeli inahusiana na dhana moja au zaidi. Utafiti wake pia ulitambua kuwa lugha za Kibantu kama vile Kiswahili na Kikikuyu zina takiriri za viambishi kwenye vipande vya sarufi.

Akichunguza athari za lugha mama (lugha za kienyeji) katika Kiswahili mkoani Mara nchini Tanzania, Massamba (1986) aligundua kuwa, lugha za kienyeji katika mkoa wa Mara ziliathiri Kiswahili kifonolojia, kimsamiati na kisarufi. Miongoni mwa athari zikiwa mabadiliko ya kimofonolojia ya kuongeza na kudondosha sauti katika matumizi ya maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha za kwanza. Utafiti wake ulitambua kuwepo kwa makosa ya kimofolojia na kimuundo kutokana na athari za uhamishaji wa viambishi mbalimbali kutoka lugha za kwanza na kuingizwa katika Kiswahili sanifu. Uhamishaji huo, ulikiuka kaida za Kiswahili Sanifu na kutatiza uwasilishaji wa ujumbe ulionuiwa.

Nyanda (2015) katika utafiti wake wa athari za Kinyamwezi katika lugha ya Kiswahili, aligundua kuwa mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti husababisha mwathiriano wa lugha jirani. Matokeo ya utafiti wake uligundua kuwa wazungumzaji wa lugha mbili zinazokaribiana wanapozungumza huwa wanadhihirisha baadhi ya tofauti katika viwango vya kiisimu vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Mudhune (1994), akichunguza ujifunzaji wa mofosintaksia ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa Kiluo kwa mtazamo wa uchanganuzi Lingashi, aligundua athari za vipashio vya mofosintaksia vya Kiluo katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Komunte (2000) katika utafiti wake wa athari za lugha za Kibantu kwa L2, aligundua kuwa wanafunzi walitumia kanuni za L1 katika ujifunzaji wa stadi za kuzungumza na kusoma katika ujifunzaji wa L2 na hivyo kuchangia matumizi yasio sahihi ya L2. Mukuthuria (2004) akishughulikia kuathiriana kwa Kiswahili na Lahaja za Kitigania, aligundua kwamba wanafunzi waliathiri tahajia na sarufi ya Kiswahili sanifu au kinyume kutokana na kuhamisha maumbo na miundo ya kiisimu ya L1 au L2 katika matumizi kutokana na mifumo ya kimofolojia na kifonolojia ya lugha ya Kiswahili na Kitigania.

Akichunguza kuhusu kuibuka kwa viswahili nchini Kenya, Munyua (2002) alitambua kuwa athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili husababisha makosa mbalimbali ya kimatumizi ambayo huchangia matumizi potofu ya lugha ya Kiswahili katika viwango vyote vya lugha. Fromkin, Rodman

na Hyams (2018), alitambua kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili kwa watu wazima hutegemea mfumo wa kisarufi wa lugha yao ya kwanza wa kuhamisha kaida za kisarufi za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa vipashio vya kisarufi vya L2. Nao Joy (2012) na Vincent, (2018), katika kuchanganua dosari za kisintaksia zinazofanywa na wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili, walibaini kuwa, wazungumzaji walichanganya ngeli za nomino za L1 kiidakho na Kiiraq katika matumizi ya nomino za Kiswahili sanifu kwa kuhamisha maumbo na ngeli nomino ambazo hutofautiana na ngeli nomino za Kiswahili sanifu na hivyo kuathitri upatanishi wa kisarufi wa tungo za Kiswahili sanifu.

Mawazo ya wataalamu hawa wote yanaonesha kuwa panapotokea mtagusano kati ya lugha moja na nyingine, lugha hizo huathiriana kisarufi kutokana na uwiano na tofauti za mifumo baina ya L1 na L2. Ni kutokana na msingi wa mawazo ya wataalamu hawa ambapo makala haya yalichunguza mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia wa ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

Utafiti huu uliongozwa na mihimili miwili ya nadharia ya Umilikifu na Unganifu ya Chomsky (1981) kama ilivyoendelezwa na (Shabani, 2015). Mhimili wa kwanza unazingatia sifa za sarufi bia ambao huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Mhimili wa pili ni wa upatanifu unaofafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Utafiti huu ulishughulikia uhusiano wa kisintaksia ambapo neno moja hutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo (TUKI, 1990) na uwakilishi ngeli kuchukua nafasi ya nomino katika sentensi kuathiri upatanisho wa kisarufi wa maumbo ya maneno mengine katika maandishi na mazungumzo ya wanafunzi (kirejeo sabaki kufungamana na kipashio kinachomilikiwa katika tungo). Uchaguzi wa nadharia hii ulitokana na madai kuwa maarifa ya kisintaksia ya mtu yanaweza kuonyeshwa kupitia njia mbili rasmi za kanuni za kimsingi ambazo hupatikana katika lugha zote (ubia wa kanuni za kisarufi) na tofauti za kimofosintaksia za kanuni miongoni mwa lugha huweza kusababisha mwingiliano wa lugha.

Data za utafiti zilikusanywa kutoka maktabani na nyanjani. Data za maktabani zilihusisha kusoma vitabu na maandishi ya kisimu kuhusu matumzi ya kanuni za ngeli nomino kimofosintaksia za Luganda na Kiswahili sanifu. Nyanjani, data zilikusanywa kupitia kwa mijarabu iliyohusisha matumizi ya lugha, uandishi na usimulizi wa insha, mijadala ya vikundi kupima mwingiliano wa kanuni katika mazungumzo, utaratibu wa usaili na uchunzaji uliandaliwa kwa walimu na wanafunzi kwa ajili ya kuchanganua kanuni na kudhihisisha athari za mwingiliano wa kimofosintaksia wa Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu katika maandishi na mazungumzo shiriki. Data ilikusanywa kutoka kwa shule za upili 15 teule, ikishirikisha wanafunzi 117 kutoka kidato cha tano na sita wanaojifunza Kiswahili na ambao L1 ni Luganda kutoka wilaya ya Kampala Uganda.

Matokeo ya Mwingiliano wa Kanuni za Kimofosintaksia wa Ngeli Nomino za Luganda katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu

Kanuni za kimofosintaksia huchunguza utaratibu au sheria za matumizi ya kipashio cha kisarufi kuegemea muundo wake kimofolojia na kisintaksia. Utafiti huu ulichunguza sheria za kimuundo za matumizi ya ngeli kimofolojia na kisintaksia, mpangilio wa matumizi ya ngeli katika utungo, utokeaji wa ngeli katika mazingira ya utungo na dhima au uwakilishaji wa ngeli husika katika tungo kuzingatia nadharia za uunganifu na umilikifu ya Chomsky, (1981). Uchunguza wa kanuni ulizingatia **uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha kanuni ambazo huunganisha matumizi ya ngeli katika utungo, na miktadha ya kimiundo ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.**

Matokeo ya utafiti yalidhihirisha mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia za matumizi ya ngeli za Luganda katika Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu ulijitokeza pale ambapo kanuni za matumizi ya ngeli za Luganda zilidhihirika katika mazungumzo na maandishi ya Kiswahili sanifu kutokana na uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya ngeli baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia wa ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu ulijitokeza hasa wanafunzi walipotambua ukuruba wa mfumo au ugumu wa kutambua kanuni mwafaka ya kutumiwa katika mazungumzo na maandishi kudhihirisha uhusiano wa kimofosintaksia wa nomino na

maneno mengine katika tungo. Utafiti huu uligundua mwingiliano wa kuhamisha, kubadilisha, Kuchanganya, kujumlisha, kuongeza na kudondosha kanuni za matumizi ya ngeli za Luganda katika Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu wa matumizi ya kanuni za ngeli za Luganda katika Kiswahili sanifu ulipotosha sifa za matumizi ya ngeli nomino za Kiswahili na kuathiri sarufi ya Kiswahili sanifu. Ufuatao ni uchanganuzi wa kanuni na mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia za ngeli za Luganda katika Kiswahili sanifu.

Mwingiliano wa kanuni ya kimofosintaksia ya uundaji wa Nomino

Kanuni hii ilishikilia kuwa: Nomino huundwa kutokana na kupachika viambishi mbalimbali vyenye sifa za kiuamilifu za mofolojia na sintaksia kwenye mizizi ya maneno katika tungo. Kupitia kwa mijadala, mazungumzo, maandishi na usaili wa wanafunzi, utafiti huu ulidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili sanifu huunda nomino zake kwa kuwekea viambishi mbalimbali kwenye mizizi ya nomino kutumia kanuni ya kimofolojia ya uundaji wa nomino. Lugha hizi hutumia viambishi amilifu kwa kuvipachika mwanzoni mwa mizizi ya nomino kuwakilisha ngeli, idadi ya umoja na wingi pamoja na upatanishi wa kisarufi unaodhihirisha mahusiano ya neno kuu katika tungo na maneno mengine kisintaksia.

Kwa mjibu wa utafiti huu, mwingiliano wa matumizi ya kanuni za kimofosintaksia za ngeli za Luganda katika Kiswahili ulijitokeza pale ambapo wanafunzi walikopa au kuhamisha viambishi ngeli vya Luganda kimofolojia na kisintaksia kuonyesha uhusiano wa neno na maneno mengine katika tungo. Hata hivyo, katika matumizi yao, mwingiliano wa viambishi vya Luganda ulijitokeza katika matumizi ya Kiswahili sanifu na hivyo kuathiri usanifu wa matumizi ya Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu ulitokana na kuwa maumbo na taratibu za mpangilio wa ngeli za Luganda na Kiswahili sanifu unaotumiwa kuonyesha uhusiano wa nomino kuu na maneno mengine katika tungo hutofautiana hata ingawa baadhi ya maumbo yanayotumika yanafanana kama inavyodhihirika katika mifano Na. (1a-1d):

(1a)

Mwingiliano	Kiswahili sanifu	Ngeli	
Mutoto muzuri	Mtoto mzuri	m-wa	[mu-ba ya Luganda]
Muwalimu murefu	Mwalimu mrefu	m-wa	[mu-ba ya Luganda]
Mupolisi/wapolisi	Polisi	m-wa	[mu-ba ya Luganda]
Mudaktari/wadaktari	Daktari	m-wa	[mu-ba ya Luganda]

(1b)

Muti mukubwa	Mti mkubwa	m-mi	[mu-mi ya Luganda]
Mukati/mugati mutamu	Mkate mtamu	m-mi	[mu-mi ya Luganda]
Muguu gubwa	Mguu mkubwa	m-mi	[gu-ga ya Luganda]

(1c)

Vitabu byangu	Vitabu vyangu	ki-vi	[ki-bi ya Luganda]
Kiatu yangu	Kiatu change	Ki-vi	[ki-bi ya Luganda]
Viatu zangu	Viatu vyangu	ki-vi	[ki-bi ya Luganda]

(1d)

Maji mangi/maingi	Maji mengi	ji-ma	[ma ya Luganda]
Mayai mangi/maingi	Mayai mengi	ji-ma	[ma ya Luganda]
Sikio kupana	Sikio pana (semantiki [ku])	ya sikio	[okutu ku...] [ku-ma ya Luganda]

Mifano hii inadhihirisha kuwa nomino za Luganda na Kiswahili sanifu hutumia viambishi awali vya ngeli kuainisha nomino kimofolojia na kisintaksia. Miundo hii ya matumizi ya viambishi hutofautiana. Tofauti zinazojitokeza ni za kimaumbo ambazo hutumika kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi wa nomino. Viambishi vilivyotumika katika tungo kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi kutokana na neno kuu viliathiri mofosintaksia ya Kiswahili sanifu kutokana na

matumizi ya maumbo wakilishi ya ngeli nomino yaliyokuwa na muundo tofauti ingawa yalika ribiana kufanana au kufanana kimatamshi au kifonimu kama ilivyo katika mifano Na. (1a- 1d).

Mwingiliano wa Kanuni ya sarufi maumbo / mofolojia ya uambishaji maneno

Kila lugha huwa na utaratibu wa uundaji wa maneno kwa kuzingatia uambishaji wa viambishi kwenye maneno na aina za maneno katika tungo. Kanuni hii huchunguza taratibu za kuongeza mofu za kisarufi kwenye mizizi ya maneno kujenga maana fulani za kisarufi za maneno husika bila kuunda maneno mapya au bila kubadilisha aina za nomino, maneno na aina za maneno, taratibu zinazohusika katika uundaji wa maneno na matumizi ya maneno katika utungo (Katamba, 2003 na Masamba na Msanjila 2003).

Uchunguza wa uamilifu wa matumizi ya maneno miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili sanifu ambao L1 ni Luganda katika tungo kujenga maana za kisarufi kuelezea dhana, idadi ya umoja na wingi na jinsi ya maneno katika utungo ulibani kuwa, Luganda na Kiswahili sanifu huainisha nomino kimfosintaksia na kisemantiki kutokana na kigezo cha mpangilio wa vijenzi vya maneno na uambishaji wa viambishi kudhihirisha uhusiano wa neno kuu na aina za maneno katika utungo. Hata hivyo, maumbo yanayotumika baina ya Luganda na Kiswahili sanifu hutofautiana (Katamba, 2003 na Habwe na Karanja, 2003). Tofauti hizi ndiyo iliyosababisha mwingiliano wa kanuni za mofosintaksia ya tungo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu kutokana na mpangilio tofauti wa ngeli na aina za maneno au nomino inayotumika katika tungo kuwakilisha idadi ya umoja na wingi, pamoja na jinsi ya upatanishi wa kisarufi wa nomino kimrejeosabaki kuwakilisha umilikifu na ufungamanisho wa neno kuu katika virai husika kama inavyojitokeza katika J3 lifuatalo:

Jedwali 1: Maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya ngeli nomino na mwingiliano wake.

Ngeli	Maumbo ya Luganda kimofolojia	Maumbo ya Luganda kisintaksia	Maumbo ya Kiswahili kimofolojia	Maumbo ya Kiswahili kisintaksia	Mwingiliano
1	(o)mu-	a-	m(u)-	a-	[Mu-a] → [m-a]
2	(a)ba-	ba-	wa-	wa-	-
3	(o) mu-	gu-	m(u)-	u-	[mu] → [m]
4	(e)mi-	gi-	mi-	i-	[mi] ↔ [mi]
5	Li; (e)ri-	li-	ji-/ø	li-	[li-umoja] [li- wingi]
6	(a)ma-	ga-	ma-	ya-	[ma] ← [ma]
7	(e)ki-	ki-	ki-	ki-	[ki] ↔ [ki]
8	(e)bi-	bi-	vi-	vi-	-
9	(e)n-	e-	n-	i-	[n-] ↔ [Ø/n]
10	(e)n-	zi-	n-	zi-	[n] ↔ [zi]
11	(o)lu-	en-	u-	u-	-
12	(a)ka-	ka-	n-	zi-	[ka-] [Ø]
13	(o)tu-	tu-	-	-	[tu-] [Ø]
14	(o)bu-	bu-	-	-	[bu] [Ø]
15	(o)ku-	ku-	ku-	ku-	[ku] ↔ [ku]
16	wa-	wa-	pa-	pa-	-
17	ku-	ku-	ku-	ku-	[ku] ↔ [ku]
18	mu-	Mu-	mu-	mu-	[mu-] ↔ [mu-]
20	(o)gu-	gu-			
22	(a)ga-	ga-			
23	E				

Kwa mjibu wa maumbo haya, utafiti huu ulitambua kuwa kuna maumbo ya Luganda na Kiswahili ambayo hufanana ingawa yanatumia nomino za aina tofauti kisemantiki. Maumbo haya husababisha

mwingiliano wa kimofosintaksia unaojitokeza katika matumizi baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu wa maumbo ulisababisha uhamishaji maumbo ya kimofosintaksia ambapo maumbo yanayopachikwa kwenye mzizi wa nomino kuwakilisha idadi ya umoja na wingi yanatofautiana hata ingawa watumiaji huyatazama kama alamofu ya mofimu moja. Kwa mfano, maumbo ya ngeli ya tatu umoja [mu] ya Luganda na [m] ya Kiswahili sanifu, ngeli ya kimofolojia ya nomino ya nne [mi] ya Luganda na [mi] ya wingi, ngeli ya tano [li] ya umoja katika Luganda na [li] ya wingi katika Kiswahili sanifu, ngeli ya kimofolojia ya sita ya umoja [ma] ya Luganda na Kiswahili sanifu, ngeli ya saba ya nomino umoja [ki] ya Luganda na Kiswahili sanifu, ngeli ya tisa ya nomino nazali za Luganda [n] umoja na [zi] ya upatanisho na ngeli ya n/ Ø ya umoja na [zi] ya wingi, ngeli ya kumi ya wanyama ya [n na zi] ya umoja na wingi ya Luganda na ngeli ya [n/ Ø] ya umoja na [zi] ya wingi isiyo ya wanyama na mwisho ngeli ya [ku na mu] ya kitenzi jina na mahali ndani. Maumbo haya yanafanana ila yanatumia nomino ambazo zinatofautiana kisemantikai kwa mjibu wa Luganda na Kiswahili sanifu.

Mwingiliano uliojitokeza nyanjani ni kuwa; wanafunzi ambao L1 ni Luganda walikopa na kuhamisha viambishi vya Luganda kimofolojia na sintaksia katika tungo virai vya Kiswahili hasa walipopata ugumu wa kuelewa viambishi mwafaka kutokana na msingi wa kimofolojia na kisintaksia wa uambishaji wa maneno katika tungo. Matumizi haya yalitokana na mfanano wa kifonolojia wa maumbo yanayowakilisha viambishi awali vya nomino na maumbo yaliyoonekana kuwa alamofu ya viambishi husika. Hali iliyoathiri usanifu wa Kiswahili sanifu, kitahajia, kisintaksia na hata kisemantiki kutokana na kutumia sifa za kimofolojia za nomino husika kudhihirisha upatanishi wa kisarufi wa nomino na maneno mengine katika tungo kama ilivyo katika mfano Na. (2a-2c).

Mfano (2):

Mwingiliano wa Luganda kwa Kiswahili		Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu	
a) Ng'ombe zimeletwa nyumbani	[n-zi]	Ng'ombe wameletwa nyumbani	[Ø-wa]
b) Mbuzi zinakula majani	[n-zi]	Mbuzi wanakula majani.	[Ø-wa]
c) Paka zimekamata panya	[n-zi]	Paka wamewakamata panya	[Ø-wa]

Wanafunzi walihamisha viambishi vipatanishi vya ngeli ya 10 ya Luganda katika matumizi ya nomino katika ngeli ya 1 na 2. Uhamishaji huu ulitokana na wanafunzi kutafsiri nomino za Luganda za wanyama na kuhamisha maumbo ya nomino husika kutoka ngeli ya 10 ya [n-zi] hadi ngeli ya 1 na 2 kisemantiki. Uhamishaji huu ulibadilisha maumbo ya upatanishi wa nomino za ngeli ya [m-wa/a-wa] hasa kwa nomino za viumbe hai ya wanyama ambayo hayabadiliki kimaumbo. Viambishi vipatanishi vya nomino za majina ya Kiswahili ya viumbe hai kama wanyama yalitumia viambishi awali vipatanishi vya nomino kutoka katika ngeli ya 10 ambayo ni ngeli ya majina ya wanyama katika Luganda. Kwa mjibu wa ngeli hii, majina ya ngeli hii yamo katika wingi na hujumuisha majina ya wanyama. Majina haya huchukua mofu dhahania ya wingi ila maumbo ya upatanishi ndiyo yanayojitokeza katika tungo kuwakilisha kanuni ya umilikifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Matumizi ya kanuni hii yalidhihirishwa kwa kutumia kiambishi awali kipatanishi [zi] badala ya kipatanishi cha Kiswahili sanifu [wa] katika mfano wa (4a na 4b). Uhamishaji huu wa maumbo ya nomino ya ngeli ya 10 ya Luganda na kuyaambisha katika nomino za ngeli ya Kiswahili yaliathiri usanifu wa Kiswahili sanifu.

Aidha, wanafunzi walitumia maumbo ya awali ya mofolojia na maumbo ya viambishi vipatanishi vya nomino vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kimazungumzo na kimaandishi na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu hasa katika maneno na tungo virai na kujenga tahajia na semantiki potofu kama katika kama katika mfano Na.(3a-3d):

Mfano (3):

Mwingiliano wa Luganda kwa Kiswahili		Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu	
a) Mukate gumeisha jokoni	[mu-gu]	Mkate umekwisha jokoni	[m- u]
b) Miti gimekatwa	[mi-gi]	Miti imekatwa	[mi-i]
c) Mugulu gunaluma	[mu-gu]	Mguu unauma/ unaniuma	[m-u]
d) Maguu gananiuma	[ma-ga]	Miguu inaniuma	[mi-i]

Mwingiliano wa Kanuni ya sarufi miundo

Uchunguzi wa mazungumzo na maandishi ya wanafunzi yalidhihirisha kuwa, mpangilio wa maumbo ya kimofolojia na kisintaksia yaliyotumika na wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda hayakuzingatia miundo ya kisarufi wa viambishi kuonyesha uhusiano wa nomino kuu na maneno mengine. Wanafunzi waliamisha viambishi vya Luganda katika maneno ya tungo za Kiswahili sanifu. Uhamishaji huu ulikiuka kanuni ya sarufi maumbo inayozingatia kuwa mpangilio wa maumbo ya kimofolojia katika kategoria ya maneno lazima yaathiri vipashio na umbo linalofuata katika muundo wa tungo. Vilevile, upatanifu wa kisarufi katika tungo lazima utawaliwe na vipashio vya kimofosintaksia vilivyo na uwezo wa kuathiriana ambapo kipashio cha kwanza hutegemea sana kipashio cha pili ili kuleta maana kama katika mifano Na. (4a-4c)

Mfano (4):

- | | | |
|--|------------------------------------|----------------|
| a) Mbuzi emepelekwa malishoni kula nyasi | Mbuzi amepelekwa malishoni | [en-a] |
| b) Mbuzi imepelekwa malishoni kula nyasi | Mbuzi amepelekwa malishoni | [i-a] |
| c) Mbuzi zimepelekwa malishoni kula nyasi | Mbuzi wamepelekwa malishoni | [zi-wa] |

Wanafunzi waliamisha maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya Luganda katika tungo za kimofosintaksia za Kiswahili sanifu. Maumbo ya tungo wa (a na c) ni maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya ngeli ya 9 na 10 ya Luganda ambayo hayaonyeshi nomino kuu kumiliki kitendo kinachotendeka wala kitendo kuathirika na nomino katika Kiswahili sanifu bali yanadhihirisha mrejeosabaki wa Luganda ambapo nomino humiliki kitendo na kitendo kumilikiwa na nomino kuu. Hali ya nomino kuathiri na kuathiriana hayajitokeza katika Kiswahili sanifu bali yamejitokeza katika Luganda kwa sababu wanafunzi waliamisha kanuni hii ya miundo sarufi kutoka Luganda hadi Kiswahili sanifu. Nomino mbuzi haidhihirishi kiambishi awali cha umoja katika Luganda na Kiswahili sanifu. Kiupatanifu au kisintaksia, maumbo ya kudhihirisha umoja na wingi yanadhihirishwa na maumbo ya viambishi awali vya vipatanishi wa kisarufi vinavyopachikwa kwenye vitenzi na maneno mengine katika tungo. Uamuzi huu wa kutumia maumbo ya Luganda **[en]** kwa umoja na **[-zi]** kwa wingi katika matumizi ya nomino za Kiswahili sanifu badala ya **[a-]** kwa umoja na **[wa]** kwa wingi kulingana na utaratibu wa uainishaji na uambishaji maumbo, yaliharibu usanifu wa maumbo yanayoonyesha mahusiano ya nomino kuu na maneno mengine katika tungo yakiwakilishwa na viambishi awali vinavyopachikwa kwenye mizizi ya nomino na vitenzi katika tungo. Hali ambayo ilienda kinyume na kanuni na kuharibu usanifu wa Lugha ya Kiswahili sanifu.

Mwingiliano mwingine ulioathiri Kiswahili sanifu ni ule wa kujumlisha maumbo ya viambishi awali vya ngeli za maneno na kuchanganya maumbo awali ya viambishi awali vya Luganda katika Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu hukuonyesha mahusiano ya karibu ya nomino kuu na maneno mengine katika tungo na hivyo kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Ujumlishaji na uchanganayaji wa viambishi awali vya ngeli ulijitokeza katika ngeli hasa zilizo na ukuruba wa kimaumbo kama vile ngeli za **[a-wa]**, **[m-mi]**, **[ki-vi]**, **[ø /ji-ma]** kama inavyojitokeza katika mifano kama katika mfano Na.(5a-5e):

Mfano (5):

Mwingiliano wa Luganda kwa Kiswahili

Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu

- | | | | |
|-------------------------------|----------------|--------------------|----------------|
| a) Wamikate gimeletwa | [wa-gi] | Mikate imeletwa | [mi-i] |
| b) Wamutoto banayimba | [wa-ba] | Wanafunzi wanaimba | [wa-wa] |
| c) Kiongozi kinaongeya | [ki-ki] | Kiongozi anaongea | [ki-wa] |
| d) Kifaru kinakimbia | [ki-ki] | Kifavu anakimbia | [ki-a] |
| e) Macho gananiuma | [ma-ga] | Macho yananiuma | [ma-ya] |

Wanafunzi walitumia kiambishi cha wingi **[wa]** katika kishazi cha (5a na 5b) kwa sababu ya kanuni ya ngeli ya kwanza ambapo wingi wa **[n]** ni **[wa]** kwa hiyo badala ya wanafunzi hawa kuitumia vyema walijumlisha tu kanuni hii na kuambisha nyuma ya viambishi vyovyote vinavyoanza na umbo **[m]**. Aidha, badala ya kutumia viambishi vya upatanishi wa kisarufi unaotokana na nomino kuu ya Kiswahili vya **[mi]** ya kimofolojia leksia na **[i]** ya upatanishi wa kisarufi katika (5a) na umbo **[wa]** la

kimofolojia leksia kuwakilisha umoja na umbo [wa] ya upatanishi wa nomino kisintaksia, walitumia viambishi vya upatanishi vya wingi kutoka L1 [wa-gi] na [wa-ba] ambayo ni Luganda sanifu. Katika mifano ya (5c –5d), wanafunzi walihamishi kanuni ya Kiswahili kuwa kila nomino inayoanza na kiambishi [ki] hubadilishwa na kuwa [vi] katika wingi. Hali hii ni ya ujumlishaji kwa sababu haikuzingatika kanuni ya majina au nomino ya viumbe hai ambao hutumia kiambishi [ki-vi] kwa umoja na katika upatanishi wa Kisarufi kutumia viambishi vya ngeli ya 1 na 2 [a-wa]. Maumbo haya ni viwakilishi vya wingi katika Luganda hata hivyo sivyo vya kiswahili na havionyeshi uhusiano wa nomino kuu ya Kiswahili na vitenzu ambapo vimeambishwa. Mfano wa (5e) unaonyesha kanuni ya kutumia viambishi katika maneno kwa sababu ya mfanano wa maumbo ya maneno katika umoja na wingi wa Luganda. Wanafunzi walihamisha kiambishi kipatanishi cha wingi [gi] kwenye kitenzi cha nomino kuu kwa sababu ya umbo la nomino [macho] ambalo linakaribiana na la Luganda ambalo ni [maaso]. Ujumlishaji na kufaninisha maumbo ya nomino pamoja na kutumia kanuni za Kiswahili sanifu visivyo katika tungo za kimofosintaksia yaliathiri matumzi ya Kiswahili sanifu kama ilivyotolewa na wanafunzi katika mazungumzo, mijadala na maandishi yao.

Mwingiliano wa Kanuni ya umiliki na usabaki wa viambajengo

Kanuni ya umiliki na usabaki ni kanuni ya sarufi miundo virai ambayo huonyesha uhusiano wa viambajengo katika tungo. Kanuni hii inashikilia kuwa: **vifundo huunda kiambajengo kama na kama tu viambajengo hivyo vitakuwa ni jozi za vifundo vinavyomilikiwa kikamilifu na kifundo kikuu** (Chomsky, 1957:1967). Aidha, katika utaratibu wa kuunganisha KN na KT, vitenzi huambishwa kwa maumbo ya viambishi vipatanishi vya nomino kuwakilisha sifa za kisarufi za mofosintaksia kuwakilisha nafsi, ngeli na idadi, ya umoja na wingi wa kiima na kitenzi. Umiliki ni uhusiano wa kisintaksia wa neno moja kutawala umbo la kimofolojia la neno au maneno mengine katika tungo. Kisabaki ni umbo linalotumika kurejelea neno lililotajwa awali au litakalotajwa baadaye (Lusekelo, 2017. Kwa mjibu wa kanuni hii umiliki na usabaki hudhihirika kupitia kwa viambishi ngeli vya nomino na vitenzi ambapo kwa msingi wa kanuni ya ufungami, kiambishi ngeli huwa ni anafora huku nomino ikiwa ni kisabaki. (Mathooko, 2004, Haegeman, 1994, ASiko, 2011, Businge, 2014).

Uchunguzi wa maandishi na mazungumzo ya wanafunzi ilibaini kuwa; wanafunzi walihamisha viambishi vya ngeli nomino vya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kudhihirisha mahusiano ya umiliki wa usabaki wa nomino na vivumishi katika tungo. Hali ambayo ilikiuka matumizi sahihi ya kanuni ya umiliki na usabaki, **neni kuu katika kirai nomino (KN) hupatana kisarufi na vivumishi vyake kuhusu vipengele kama vile ngeli, idadi ya umoja na wingi na nafsi**. Matumizi ya maumbo ya Luganda ambayo hayawezi kuonyesha umiliki na usabaki wa nomino kuu na vivumishi vya Kiswahili huathiri matumizi ya Kiswahili sanifu katika maandishi na mazungumzo kama katika mfano Na.(6a-6e):

Mfano (6):

- | | |
|---|---|
| a) Muwalimu muzuri o napenda wewe. | Mwalimu mzuri anakupenda.[mu-m] |
| b) Mayai mangi/maingi gamepasuka. | Mayai mengi yamepasuka. [ma-me] |
| c) Maji Mangi/ maingi imemwagika. | Maji mengi yamemwagika. [ma-me] |
| d) Bikapo bikubwa by angu bi napendeza. | Vikapu vikubwa vyangu vinapendeza.[bi-v] |
| e) Byatu byangu zimeribika. | Viatu vyangu vimeharibika. [by-vi] |

Mifano hii inadhihirisha ukiukaji wa maumbo ambayo yanafaa kuambisha kwenye nomino na vivumishi kuonyesha uhusiano wa nomino na vivumishi. Maumbo ya nomino yaliyotumika katika [a-e] ni maumbo ya Luganda ambayo hayadhahirishi kanuni ya umiliki na usabaki wa nomino kuu na vivumishi katika tungo. Hii ni kwa sababu maumbo yaliyotumika na wanafunzi hayakuwa maumbo ya kifonolojia ya ngeli ya Kiswahili sanifu yanayostahili kuambishwa kwenye nomino na vivumishi kudhihirisha nomino kumiliki kivumishi na kivumishi kumilikiwa na nomino kupitia kwa maumbo. Hii inatokana na kanuni kuwa viambishi vinavyokaririwa katika nomino ndivyo vinavyokaririwa katika vivumishi katika tungo, kanuni ambayo ilikiuka na wanafunzi katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Wanafunzi walihamisha maumbo ya Luganda katika matumizi ya nomino na vivumishi vya

Kiswahili, kushidwa kutambua kanuni za kimofofolojia zinazotokea katika baadhi ya viambishi awali vya nomino [b na c] Kwa mfano walitumia kivumishi [maingi] jinsi kilivyo bila kutambua mabadiliko ya kifonolojia, ambapo [a + i] huunda fonimu mpya /e/ na badala yake kutumia aidha kivumishi jinsi kilivyoambishwa au kutumia maumbo ya Luganda [mangi] katika Kiswahili sanifu.

Mwingiliano mwingine ulioathiri matumizi ya ngeli za Kiswahili sanifu ni ule wa kujumlisha na kuchanganya kanuni za matumizi ya nomino za mkopo zinazojitokeza katika Kiswahili sanifu ambazo zimeainishwa katika ngeli ya kwanza. Nomino hizi kulingana na uainishaji wa Mgullu (1999) hutumia umbo kapa [ø] kwa umoja na umbo [ma] kwa wingi kimofolojia. Hata hivyo, wanafunzi Walitumia maumbo ya kimofolojia ya Luganda katika nomino hizi za Kiswahili sanifu kuwakilisha maumbo ya nomino hizi kwa umoja na kuchanganya maumbo ya kisintaksia ya Luganda ya nomino hizi kuwakilisha miundo ya nomino hizi kwa wingi kama katika mfano Na.(7a-7f):

Mfano (7):

Mwingiliano wa Luganda kwa Kiswahili

- | | |
|------------------------------|-----------|
| a) Mupolisi alikuja hapa | [mu-a] |
| b) Wapolisi walikuja hapa | [wa-wa] |
| c) Musirikari amekamata mutu | [mu-a/ba] |
| d) Waaskari wamekamata mutu | [wa-wa] |
| e) Wadaktari wanatibu sisi | [wa-wa] |
| f) Waaskari wamekamata mutu | [wa-wa] |

Maumbo sanifu ya Kiswahili sanifu

- | |
|-------------------------|
| Ø-polisi alikuja hapa |
| Mapolisi walikuja hapa |
| Askari amekamata mtu |
| Maaskari wamemshika mtu |
| Madaktari wanatutibu |
| Maaskari wamemshika mtu |

Mifano hii inadhihirisha matumzi ya maumbo ya umoja [mu] yanayotumika katika Luganda katika sentensi ya umoja na kujumlisha kanuni ya kutumia kiambishi [wa] ya Kiswahili ya viumbe wenye uhai katika ngeli ya [wa] ambayo hupatikana katika ngeli ya 1 na 2 [mu-wa/a-wa] katika kuambisha nomino hizi kwa wingi badala ya kiambishi sahihi [ma-] kama ilivyostahili kutumika. Mwingiliano huu uliathiri matumizi ya Kiswahili sanifu kwani uliweza kupotosha umiliki na usabaki wa nomino kuu na maneno mengine katika tungo. hali hii ilipotoshi umantiki na usarufi wa Kiswahili sanifu kimatumizi.

Mwingiliano wa Kanuni ya kifonolojia ya udondoshaji

Sauti za lugha zinapotumika katika neno au tungo, mara nyingi huweza kuathiriana na kusababisha msuko wa sauti zinazolingiliana. Kanuni za kifonolojia ni kanuni zinazohusika na matamshi ya mofimu zinazojenga maneno. Kanuni hizi huhusika zaidi na mabadiliko ya matamshi ya mofimu kutokana na mkabiliano wa mofimu.

Ngeli za Luganda na Kiswahili zimeundwa kwa maumbo ya kimofofonolija ambayo matumzi yake yasipizingatiwa kimaandishi na Kimazungumzo, sifa za lugha husika huathirika na kupoteza usanifu wake. Kwa mjibu wa kanuni hii, utafiti huu ulitambua kuwa wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda waliamhisha matamshi ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili, kubadilisha sauti kwa mjibu wa L1, kushindwa kutambua kanuni za kimofosintaksia zinazoongoza baadhi ya maneno na kuyatumia jinsi yalivyo katika tungo za Kimofosintaskia za Kiswahili sanifu. Hali hii ilipotosha usahihi wa matumzi ya Kiswahili sanifu kwa sababu sauti zenyewe zilikiukwa kimaandishi na kimatamshi kama katika mfano Na.(8a-8h):

Mfano (8):

Matamshi na maandishi

- | | |
|--|-------------------------------------|
| a) Watoto w-[a-i]-ngi walikuja darasani. | Watoto w-[e]-ngi walikuja darasani. |
| b) Mayai m-[a-i]-ngi yameoza. | Mayai M-[e]-ngi yameoza. |

Ubadilishanaji sauti badala ya [wa]

- | | |
|---|---|
| c) Wapolisi walibakamata w[-a-i]-zi.[-ba-] | Mapolisi wali-[wa]-kamata w-[e]-zi [-wa-] |
| d) Leta vitu [mu]-[bi]-ingize ndani.[mu-, -bi-] | Leta vitu [m]-[vi]-ingize ndani. [m-vi-] |

Kubadilisha matamshi ya viambishi; mofimu [ki-] na kutumia [ch] na [cha] kuandikwa kama [kya], [che] kuandikwa kama [kye]

- | | | |
|--------------------------------|---------------------------|---------|
| e) [Kya]-kula chimeiva chilete | [Cha]-kula kimeiva kilete | [ky-ch] |
|--------------------------------|---------------------------|---------|

f) [Chi]-kombe [kye]-usi [chi]-mepasuka [Ki]-kombe [che]usi [ki]-mepasuka.

Kukiuka kanuni ya kudondosha fonimu [-u] inayofuatwa na konsonanti

g) [Mu]-kate [mu]-zuri. Mkate [m]-zuri.

h) M [-u]-walimu muzuri. [Mw]-alimu [m]-zuri.

Wanafunzi walidhihirisha ukiukaji wa kanuni ya kimofonolojia kwa kuandika na kutumia mofimu ya viambishi vipatanishi vya kimofosintaksia vya Luganda katika mazungumzo na maandishi ya Kiswahili sanifu. Vivumishi vingi vilipokea ukiukaji wa kanuni za kimofosintaksia kama vile katika [a, b, c, na f]. katika ubadilishanaji wa sauti, wanafunzi walihamisha mofimu za viambishi vinavyoakaribiana kimaumbo, kimatamshi na kiuanishaji ya Luganda na Kuitumia katika kiswahili sanifu. Kwa mfano katika [c-h]. Matumizi haya yalionyesha ukiukaji wa matumizi ya maumbo sahihi na matamshi sahihi ya viambishi vya ngeli nomino ambavyo vimejegwa kimofonolojia kuwakilisha idadi ya umoja na wingi wa nomino kuegemea sifa za Kiswahili sanifu. Ukiukaji huu ulisababisha athari za kimofosintaksia za tahajia na maendelezo yanayoonyesha matumizi mabaya ya Kiswahili sanifu.

Mwingiliano wa Kanuni ya kisarufi ya matumizi ya vibainishi na viambishi katika utungo

Kanuni hii hushikilia kuwa; viambajengo huwa katika sehemu tofauti za neno na katika mkutadha wa utungo na vinaunganishwa na sheria fulani ambazo husababisha umilikifu na uunganishaji wa viambajengo hivyo kuwakilisha idadi na jinsi ya kisarufi ya umoja na wingi kimofosintaksia. Hii ina maana kuwa kimuundo matumizi ya vibainishi na viambishi nomino katika utungo lazima vibebe taarifa za kisarufi za nomino katika utungo kimofosintaksia. **Taarifa hizi ni seti za kisarufi za idadi, nafsi, uhusika, ngeli, dhamira [maana], na jinsi ya nomino katika utungo.** Matumizi haya lazima yazingatie maumbo ya kimofolojia na kisintaksia ya maumbo kamili ya ngeli ambamo nomino kuu huainishwa. Kila lugha huainisha ngeli zake kutumia maumbo wakilishi ya dhima za kisarufi. Maumbo haya yakikiukwa, dhima ya uambishaji wa nomino husika hupotoka na hivyo usanifu wa Lugha pia kupotoka kwa sababu dhima ya kueleza seti za kisarufi za matumizi ya vibainishi na viambishi husika katika kategoria za kisarufi katika tungo zimekeukwa. Kanuni hii huongozwa na kanuni ya viambajengo vya nomino katika utungo na kanuni ya dhima ya viambajengo katika tungo

Kimatumizi, utafiti huu uligundua kuwa wanafunzi ambao L1 ni Luganda hutumia maumbo ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kuwakilisha seti za kisarufi za ngeli, idadi ya nomino kwa umoja na wingi, dhamira, jinsi ya kisarufi ya upatanishi wa kisarufi wa nomino kuu na maneno mengine katika tungo kama katika mfano Na.(9a-9f):

Mfano (9):

a) **Katoto** kanasumbua mimi **Mtoto** ananisumbua
b) Ona **bunyama** wewe napea mimi Tazama nyama **chache** uliyonipa

Tazama **vipande vidogo** vya nyama ulivyonipa

c) Baba ameyingia **mu** nyumba Baba ameingia chumbani.
d) **Muwalimu** ameyenda ekampala Mwalimu ameenda Kampala.[e- Mahali (Kampala)]
e) We ulimupa chakula **mingi** Umenipa chakula **kingi**
f) Mbuzi **yange** imepotea Mbuzi **wangu** amepotea

Mifano hii inadhihirisha matumizi yaliyokiuka kanuni ya kisarufi ya matumizi ya viambishi ngeli kuwakilisha upatanishi wa kisarufi katika tungo. Wanafunzi kwa mfano, katika kueleza dhima ya udogo wa [mtoto] katika [a na b-] badala kutumia viambishi vya Kiswahili sanifu vya ngeli ya [a na 2] walitumia ngeli ya 13 na 14, kuwakilisha dhima ya kudhalalisha nimono. Ngeli hii hautumiki katika Kiswahili sanifu kwa sababu ya itikadi ya kuheshima na kudhamini binadamu. Katika [d] wanafunzi walitumia kiambishi cha Luganda [e-] kuwakilisha mahali na katika [d] wakatamia [mu] kuwakilisha mahali ndani. Katika c), wanafunzi wahamisha viambishi vya nafsi ya pili umoja [m] na kiambishi [mi] cha idadi kisichozingatia uambishaji wa nomino za Kiswahili sanifu katika kutumia

Kiswahili sanifu. Katika f), wanafunzi wametumia kiambishi cha Luganda cha vivumishi [y-] nafsi ya kwa nza umoja badala ya kiambishi sahihi cha Kiswahili sanifu [w].

Hitimisho

Kwa kuhitimisha, Uchunguzi wa utafiti huu ulidhihirisha mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia za Luganda katika Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu ulijitokeza katika matumizi ya kanuni za ngeli za Luganda Katika Kiswahili sanifu. Wanafunzi wa Kiswahili ambao L1 ni Luganda walihamisha, kuchanganya, kudondosha, kuchepeka au kuongeza viambishi kutokana na kuhamisha kanuni, kujumlisha, kubadilisha utaratibu wa kisemanti, mofolojia na sintaksia kwa kanuni za matumizi ya ngeli za Luganda katika matumizi Kiswahili sanifu. Mwingiliano huu ulijitokeza katika uambishaji wa maumbo ya uwakilishi wa nomino na maneno mengine katika tungo kuonyesha seti za kiisimu za kimofosintaksia zinazoeleza upatanishi wa kisarufi wa idadi ya wingi na umoja, nafsi, uhusika, ngeli, dhamira [maana], na jinsi ya nomino katika utungo. Mwingiliano huu ulisababisha athari za kisarufi za Kiswahili sanifu na kujenga lugha kadri isiyo Kiswahili sanifu kimaumbo, kisarufi, kidhima, uhusika, ngeli na idadi ya umoja na wingi. Uchunguzi huu vilevile ulitambua kuwa ukuruba na tofauti za maumbo na seti za kutambulisha matumizi ya ngeli nomino kuwakilisha upatanishi wa kisarufi wa neno kuu na maneno mengine katika tungo kimofosintaksia ndizo zilizochangia mwingiliano huu. Hii ni kwa sababu seti hizi zilikuwa moja ila zilitofautiana kimaumbile na kimatumzi kutegemea sifa na kanuni za lugha.

Makala haya yalichunguza mwingiliano wa kanuni za kimofosintaksia wa ngeli za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu ukijikita katika kipashio cha ngeli. Kuna mambo mengine yanayoweza kuchunguzwa kuhusiana na ngeli za lugha hizi mbili na vipashio vinginevyo vinavyohusiana na lugha hizi mbili. Aidha, utafiti mwingine unaweza kufanywa katika lugha zingine na Kiswahili na kudhihirisha mwingiliano au jinsi vipashio vya L1 vinavyochangia na kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu.

Marejeleo

- Asiko, B. A. (2011). Uamilishi Dhima katika Sentensi za Luloogoli: Mtazamo wa sintaksia Finyizi.
- Businge, J. (2014). *Uchanganuzi wa Kimofosintaksia wa Sentensi za Kitooro kwa Mkabala wa Nadharia ya Umilikifu na Unganifu*. Chuo Kikuu cha Uisilamu Mbale, Uganda.
- Chomsky, N. (1957). Fundamentals of Language.
- Chomsky, N. (1967). Logical structures in language. *American Documentation (pre-1986)*, 8(4), 284.
- Chomsky, Noam. (1981). Lectures on government and binding. Dordrecht: Foris.-. 1986. Knowledge of language: Its nature, origin, and use. *New York: Praeger..(1993)" A Minimalist Program for Linguistic Theory". Kenneth Hale and Samuel J. Keyser, Eds. The View from Building, 20, 1–52.*
- Fromkin, V., Rodman, R., na Hyams, N. (2018). *An introduction to language*. Cengage Learning.
- Habwe J. na Karanja P. 2004. *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Haegeman, L., na Atkinson, M. (1994). *Introduction to Government and Binding Theory 11* (second edi). Malden, Massachusetts: Blackwel Publishers Ltd.
- Hyman, L. M., na Katamba, F. X. (2001). November, 2001 The Word in Luganda Larry M. Hyman. *Word Journal Of The International Linguistic Association*, (1).
- Joy, M. S. (2012). Causes of syntactical errors in Kiswahili second language learning among western Kenya's Kiidakho first language speakers. *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies*, 3(6), 921.
- Kapinga, MC. (1983). Sarufi Maumbo ya Kiswahili sanifu. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Katamba, F. (2003). Nominal Morphology. In Derek Nurse, Gérard Philippson (eds.) *The Bantu languages*, Routledge., 103–120.
- Katamba, F. X. (2006). Uganda: The language situation.
- Kihore, Yared M, Massamba, D. P. B., na Msanjila, Y. P. (2001). Sarufi Maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA). *Sekondari Na Vyu. Dar Es Salaam*.

- Kihore, Yared Magori, Massamba, D. P. B., na Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA): sekondari na vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- Komunte, B. S. (2000). The Impact of Bantu Languages in English Language Learning Processes in Tanzania Secondary Schools. *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili*, 2000, 287 – 296.
- Lusekelo, A. (2017). The Swahili noun phrase in its Sentential: Katika *Mkwawa Journal of Education and Development*, *Juzuu 1, Issue 1, 2017*: DOI: <https://doi.org/10.37759/mjed.2017.1.1.3>
- Massamba, D. P. (1986). On the influence of local languages on Kiswahili: the case of Mara Region in Tanzania. *Kiswahili*, 53(1-2), 67-83.
- Mathooko P.M (2004) *Morphology and Syntax*, Nairobi: Institute of Open and Distance Learning, Kenyatta University.
- Mgullu, R. S. 1999. *Mtala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mudhune, D. R. (2008). *Athari za Kifonolojia kwa Wasemaji wa Dholuo Wanaojifunza Kiswahili*.Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Mukuria (1989). Mpangilio wa Ngeli: Ulinganishi wa Ngeli za Kiswahili sanifu na Kikikuyu cha Kiambu. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mukuthuria, Mwenda. (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahilina Kimeru: Mfano Kutokana na wanafunzi wa Tigania , Kenya*. Chuo Kii Cha Egerton.
- Munyua, J. G. (2002). The Emerging Viswahili and Kiswahili Research. Katika K. I. Simala (Mh.) *Jarida la Utafiti wa Kiswahili* (kur. 97 – 107). Eldoret: Moi University Press.
- Nyanda, J. (2015). Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili. The Open University Of Tanzania.
- Odeo, I. na Maina, G. 2008. *Fani ya Isimu Jamii kwa shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University press.
- Ontieri, J. O. (2010). *Uchanganuzi wa Makosa katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Nakuru, Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu Cha Egerton, Kenya.
- Ontieri, J. O. (2016). Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kwanza katika Kiswahili: Mfano wa Lugha Teule za Kibantu Nchini Kenya.
- Shabani, A. N. na R. (2015). Nadharia ya Utawala na Ufunganisho Inavyojihusisha na Aina za Vikundi Nomino katika Kiswahili, (2004), 1–8.
- TUKI (1990). Kamusi ya Isimu na Lugha. 1990. Dar es Salaam: TUKI. *Dar Es Salaam*:
- Vincent, S (2018). Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wairaki: Tathimini ya Dosari na Sababu za Dosari. Katika: Jarida La *UTAFITI*, Juzuu la, 13(1).